HOTUBA YA MGENI RASMI KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA USAFI DUNIANI TAREHE 15 SEPTEMBA, 2018

Mheshimiwa Makamu mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa,

Waheshimiwa Madiwani mliopo hapa

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa

Wakuu wa Idara na Vitengo na taasisi zilizopo Mpwapwa

Ndugu Viongozi wa Kata na Vijiji

Wageni waalikwa na wananchi kwa ujumla

Mabibi na Mabwana

Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku hii ya leo ya maadhimisho ya siku ya Usafi Duniani tukiwa buheri wa afya. Pili nimkushukuru sana Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mpwapwa na timu yake, kwa kunialika kujumuika nanyi katika maadhimisho haya ya siku ya Usafi Duniani leo tarehe 15/09/2018. Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wenyeji wetu uongozi wa Hospitali ya wilaya ya Mpwapwa kwa kuruhusu maadhimisho haya ya kihistoria kufanyika kwa mara ya kwanza hapa wilayani. Aidha napenda kuwashukuru watu wote mliofika katika maadhimisho haya, nawashukuru na kuwapongeza sana.

Ndugu wananchi,

Maadhimisho ya siku ya Usafi Duniani yanafanyika tarehe 15/09 kila mwaka, siku hii imeasisiwa miaka 10 iliyopita. Kwa Tanzania maadhimisho haya yanafanyika kwa mara ya kwanza mwaka huu 2018.

Ujumbe wa mwaka huu wa siku ya Usafi kidunia ni **“SIKU MOJA, SAYARI MOJA, LENGO MOJA”,** Ujumbe huu unatuhamasisha sisi sote kuungana katika kupambana na changamoto ya uchafuzi wa mazingira utokanao na utunzaji mbaya wa taka ngumu na kuifahamisha dunia kuwa suala la usafi wa mazingira ni jambo nyeti kwa afya, ustawi na maendeleo ya kila mtu kwa maendeleo endelevu.

Ujumbe wa mwaka huu kitaifa ni **“FUNGUA MACHO YAKO KUTOKA KWENYE UPOFU WA TAKATAKA NA KUWA SULUHISHO SIO UCHAFUZI”**. Ujumbe huu unatuhamasisha kuwa na urafiki endelevu na mazingira ambapo kila mtu anapaswa kutambua, kufurahi, kujivunia na kulinda uzuri wa mazingira. Hivyo hatunabudi kutimiza wajibu wetu ipasavyo kama jamii kwa kuhakikisha kuwa shughuli tunazozifanya za uzalishaji mali na utoaji wa

huduma zinakuwa rafiki wa mazingira na zisiwe chanzo cha uchafuzi wa mazingira.

Ndugu wananchi,

Afya, ustaarabu na ustawi wa taifa letu kwa ujumla vinategemea sana hali mazingira yanayotuzunguka, leo hii uchafuzi wa mazingira kwa taka ngumu umekuwa changamoto katika miji yetu ambao unazidi kuongezeka siku hadi siku kutokana na ongezeko kubwa la tabia hatarishi za utupaji holela wa taka ngumu juu ya uso wa nchi. Uchafuzi wa mazingira unaathari kubwa kiafya hasa katika uenezwaji wa magonjwa ya mlipuko, mbali na athari za kiafya serikali inatumia gharama kubwa katika uwekaji wa miji safi.

Mazingira safi ni maisha yetu, mazingira safi ni uhai wetu, mazingira safi ni afya yetu, mazingira safi ni uchumi wetu hivyo kila mmoja wetu ajitafakari namna anavyoweza kuwa na mchango chanya katika kuyaweka mazingira yetu katika hali ya safi.

Ndugu wananchi,

Kwa miaka zaidi ya 50 iliyopita nchi yetu ilikuwa na idadi ya watu inayokadiliwa kuwa Milioni 9, leo idadi ya watanzania inakadiliwa kufikia zaidi ya Milioni 50, hii itukumbushe kuwa kwa kadri watu wanavyoongezeka ndivyo uzalishaji wa taka ngumu unavyoongezeka na hivyo kuongeza changamoto ya utunzaji wa mazingira kutokana na uchafuzi wa mazingira kwa taka ngumu zinazotokana na ongezeko la shughuli za uzalishaji na utoaji wa huduma.

Ndugu wananchi,

Ifahamike kuwa gharama za uchafuzi wa mazingira ni kubwa sana ukilinganisha na gharama za kudhibiti uchafuzi. Kwani baadhi ya gharama za uchafuzi wa mazingira baadhi yetu tumekwisha kuzipata mfano:- kuwapoteza wapendwa wetu kwa magonjwa yanayotokana na uchafu (Kuhara damu, Malaria n.k), kuongeza gharama za maisha katika kupata huduma za kiafya pale mwanafamilia anapougua magonjwa yanayotokana na uchafu pesa ambazo zingetumika kwa shughuli za maendeleo

Kutokana na madhara ya uchafuzi wa mazingira hatuwezi kusubiri miaka iendelee kwenda pasipo kujadili, kuamua na kushiriki kusitisha uchafuzi na kutokufumbia macho pale tunapoona baadhi yetu wanapuuza adhima njema ya kuweka mazingira yetu safi. Kila mmoja wetu aamue sasa kuwa suluhisho kwa kubadili tabia ya uchafuzi na kuwa sehemu ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira kwa maendeleo yetu na vizazi vijavyo.

Ndugu wananchi,

Natambua kuwa zipo baadhi ya changamoto katika utekelezaji wa zoezi la kuweka wilaya yetu safi, baadhi ya changamoto hizo ni uchakavu wa magari ya kusomba taka ngumu, uchangiaji hafifu wa ada ya usombaji wa taka ngumu na utayari mdogo wa wanachi kubadili tabia ya kuacha tabia ya uchafuzi wa makusudi wa mazingira. Lakini kwa pamoja changamoto hizi ni rahisi kuziondoa kwa kila mtu akitimiza majukumu katika eneo lake.
Hata hivyo hatutasita kufanya maamuzi magumu pale itakapolazimu ili kusaidia kuharakisha zoezi la kuweka wilaya yetu katika hali ya usafi hasa kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaopuuza masula ya usafi wa mazingira .

Ndugu wananchi,

Ikumbukwe kuwa katika kusukuma suala la usafi wa mazingira Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa John Pombe Magufuli** aliitangaza kila jumamosi ya mwisho wa mwezi kuwa itakuwa ni siku maalumu ya usafi wa mazingira kwa nchi nzima, na kuagiza wananchi wote kufunga biashara na kushiriki kufanya usafi katika maeneo yao ya kuishi, bishara, kijamii na maeneo ya wazi. Hivyo napenda kuchukua nafasi hii kusisitiza tena wananchi wote kuona umuhimu na kulipa uzito suala la usafi wa mazingira kwa ustawi wilaya yetu. Aidha naziomba na kutoa wito kwa taasisi za kifedha na mashirika mbalimabali kuendelea kushiriki katika kampeni ya kuweka wilaya na mji wetu wa mpwapwa katika hali ya usafi.

Ndugu wananchi,

Kwa kuhitimisha napenda kuwashukuru tena na kuwapongeza sana wale wote ambao wameshiriki kuandaa maadhimisho haya ya siku ya Usafi Duniani na wale walioshiriki katika kufanya usafi. Nazipongeza taasisi zote binafsi na taasisi za umma, taasisi za dini, Vikundi na watu binafsi kwa ushiriki wenu mkubwa na dhati katika kufanikisha maadhimisho haya yanayoadhimishwa kwa mara ya kwanza hapa wilayani, natoa shukrani za kipekee kwa Benki ya NMB kwa ushiriki mzuri katika maadhimisho haya kwa kusaidia vifaa vya usafi.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

“FUNGUA MACHO YAKO KUTOKA KWENYE UPOFU WA TAKATAKA NA KUWA SULUHISHO SIO UCHAFUZI”.